(e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(f) Soksi jozi mbili nyeupe za shule
(g) Sweta rangi ya kijivu yenye “V” shingoni.
(h) Magauni mawili (2) rangi ya damu ya mzee (maroon) marefu hadi kwenye kiwiko cha mguu yenye marinda ya kufuatana yatakayovaliwa siku za Jumamosi na Jumapili na baada ya masomo. Hutaruhusiwa kuvaa nguo nyingine kinyume na hizo. Huruhusiwi kuja na sweta, jacketi au koti la aina nyingine yoyote.
(i) Wanafunzi wa Kiislam wanaruhusiwa kuvaa juba jeupe lisiwe na urembo wowote wakati wote wakiwa shuleni ( zisipungue nne)
(j) T /Shirt 2 nyeupe zisizo na maandishi wala mchoro (shingo iwe ya mduara)
(k) Raba za michezo rangi nyeupe
(l) T-shirt ya rangi ya njano ***form six*** kwa ajili ya kutokea. Kama utaikosa T-Shirt hiyo maeneo unakoishi zinapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/=
(m) Truck suit mbili rangi ya damu ya mzee (maroon)
NB: vifaa vyako vyote andika majina yako yote kwa maandishi yasiyofutika

**5.2 Michango**

**Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

*i. Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=*
*ii. Tahadhari 5,000/=*
*iii. Nembo 5,000/=*
*iv. Kitambulisho cha shule 5,000/=*
*Jumla 80,000/=*

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba **40301200137** jina Mawenzi Sekondari MMC katika Benki ya NMB ( **tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).**

**(a) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni :-**

i. Ream ya karatasi (A4) Mbili (2) kwa mwaka.
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iii. Scientific calculator na Mathematical set (kwa tahasusi za HGE na EGM.
iv. Shuka mbili za rangi ya blue.
v. Bed cover moja nyeupe isiyo na urembo wa aina yoyote
vi. Chandarua nyeupe (mosquito net)
vii. Blanketi moja rangi yoyote.
viii. Nguo ya kulalia (nightdress)
ix. Kanga / kitenge jozi MOJA TU. Mitandio na vitambaa vya kichwa haviruhusiwi.
x. Taulo, mswaki, malapa ya bata au umoja na **si vinginevyo**.
xi. Vyombo vya chakula ( sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
xii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
xiii. Sanduku MOJA la bati na begi dogo la kubebea vitabu vya darasani
xiv. Sendos nyeusi zenye uwazi mbele na kamba ya kufungia nyuma zisiwe na kisigino.

**TANBIHI:** Mwanafunzi aje na barakoa na vitakasa mikono vya kutosha

**VIFAA VYA USAFI**

| S/N | HGK | HGL | HKL | EGM | HGE |
|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Fagio refu la chelewa | Fagio la kuondoa buibui (cobwerb remover) | fagio la chelewa | Fagio refu la chelewa | Fagio refu la chelewa |
| **2.** | Panga | Sabuni ya maji lita 5(DeXi) | Dawa ya chooni lita 5 | Soft broom | Hard broom |

